



Hapo zamani,
Ngurumo na Radi
waliishi duniani
miongoni mwa watu.



Ngurumo alikuwa mamake Radi.



Radi alikuwa
mwenye hasira kali.

Mara nyingi
alibishana na
mamake.



Radi alipokasirika,
aliteketeza nyumba
na kung'oa miti.


Alitoa sauti ya
kutisha, "Pia-la-la-la,
piala- la-la!"

Aliyaharibu
mashamba na hata
kuwaua watu.




Radi alipofanya vitendo hivi, mamake alimwita kwa sauti ya juu, “Bumrambo-la-la-la, la-bum!”

Alijaribu kumzuia asisababishe uharibifu.




Radi hakutia
maanani aliyosema
mamake.

Badala yake
angesababishia kila
mmoja fujo
alipokuwa na hasira.



Hatimaye, watu walipeleka malalamishi yao kwa mfalme.




Mfalme aliamrisha
Ngurumo na
mwanawe wahame
kutoka kijijini.

Aliwafukuza waende
kuishi mbali na
makao ya watu.



Hili halikusaidia sana. Radi alizidi kuteketeza misitu alipokasirika, “Pia-la-la-la, pia-la-la-la!”

Wakati mwingine, ndimi za moto zilisambaa na kuunguza mashamba.




Kwa mara nyingine,
watu Walienda kwa
mfalme
kumlalamikia.



Mara hii, mfalme aliwaambia Radi na Ngurumo kwamba hawangeendelea kuishi duniani.

Aliwafukuza waende kuishi angani wasikoweza kusababisha uharibifu mwingi.



Tangu wakati huo,
Radi anapokasirika,
huweza kuteketeza
na kuharibu, “Pia-la-
la-la, pia-la-la-la!”

Nasi bado
tunamsikia
Ngurumo, mamake
Radi, akimkemea,
“Bum-rambola-la-la,
la-bum!”